**ARUSHA MEAT COMPANY LTD**
P.O.BOX 14167
ARUSHA
TANZANIA
TEL: +255272970304
Mob: +255734026767
E-mail: arushameatcompany@yahoo.com

**KUMB. NA. AMCL/MTNZ/78/78** **DATE: 12/09/2025.**

# TANGAZO LA NAFASI YA KAZI.

Arusha Meat Company Limited ni Kampuni iliyosajiliwa kwa mujibu wa sheria za Makampuni ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo inajishughulisha na huduma ya uchinjaji wa ng'ombe, mbuzi na kondoo. Aidha Kampuni hii pia huchakata nyama kwa ajili ya kutengeneza bidhaa mbalimbali. Arusha Meat Company Limited inakaribisha waombaji wenye sifa za kujaza nafasi tatu (3) zilizowazi kama ifuatavyo:-

## 1.0 MHASIBU MSAIDIZI (ACCOUNTANT) NAFASI MOJA (1).

### 1.1 MAJUKUMU YAKE YATAKUWA IFUATAVYO;-

i) Kupokea na kulipa fedha.
ii) Kutunza daftari la kumbukumbu za fedha.
iii) Kufanya usuluhisho wa hesabu za benki.
iv) Kupitia malipo kulingana na kanuni za fedha.
v) Kufanya jukumu jingine lolote utakalopangiwa na Meneja Mkuu kwa kushirikiana na Mkuu wa Idara.

### 1.2 SIFA ZA MWOMBAJI.

Awe na Astashahada ya Sayansi ya jamii au Sanaa kutoka katika vyuo vinavyotambuliwa na serikali na kujiimarisha (major) katika moja wapo ya fani zifuatazo:

i) Awe amehetimu cheti cha uhasibu kutoka Taasisi inayotambulika.
ii) Awe na Ujuzi wa kompyuta
iii) Uelewa wa msingi ya uhasibu.
iv) Awe na uwezo wa kuandaa na kuingiza taarifa za kifedha

v) Awe na uwezo wa kushughulikia vitabu vya hesabu.

**2.3 MSHAHARA.**

Kwa kuzingatia ngazi ya mishahara ya Arusha Meat Company Limited yaani ngazi ya **AMCL 1.**

**2.0 MCHUNAJI (SKINNERS) NAFASI MOJA.**

**2.1 MAJUKUMU YAKE YATAKUWA KAMA IFUATAVYO:-**

Kupokea ng'ombe, mbuzi, kondoo kutoka zizini/stoo kwa ajili ya kuchinja.

i) Kumwandaa ng'ombe, mbuzi, kondoo katika hatua ya uchinjaji.

ii) Kumsafisha ng'ombe na kumtundika/kumninginiza tayari kwa hatua ya uchunaji baada ya kuchinjwa.

iii) Kuchuna ng'ombe, mbuzi, kondoo kwa kuzingatia uchunaji sahihi usioharibu nyama wala ngozi.

iv) Kutengenisha ng'ombe, mbuzi, kondoo katikati ili kuondoa ogani za ndani na kuzipeleka kwenye chumba maalum iliyotengwa na Kampuni.

v) Kuweka alama ya nteja husika kwenye masalia yote ya ng'ombe, mbuzi, kondoo husika kwa usahihi ili kuongeza ufanisi na kuepusha kuchanganya bidhaa za wateja wa Kampuni.

vi) Kuhakikisha eneo la kazi ni safi wakati wote wa kazi.

vii) Kushiriki kufanya usafi wa jumla kwa siku zilizowekwa na uongozi wa Kampuni.

viii) Kutekeleza majukumu mengine ya kazi kama atakavyoelekezwa na wasimamizi wa kazi.

**2.2 SIFA ZA MWOMBAJI.**

i) Awe na leseni ya uchunaji inayotolewa na Wizara ya Mifugo.

ii) Awe anajua kusoma na kuandika kwa ufasaha.

iii) Awe na umri kuanzia miaka 21-35

**2.3 MSHAHARA.**

Kwa kuzingatia ngazi ya mishahara ya Arusha Meat Company Limited yaani ngazi ya **AMCL 1.**

## 3.0 MCHAKATAJI NYAMA (MEAT - PROCESSOR) NAFASI MOJA.

### 3.1 MAJUKUMU YATAKUWA KAMA IFUATAVYO:

Kutenganisha nyama na mifupa.

i) Kucharanga mifupa tayari kwa kuuzwa dukani, kutayarisha mikato ya nyama mfano Primecut, Back kwa mikato T-bone steak, shin kwa mikato ya ossobuco,sirloin,beef fillet pamoja na nyama za kutengeneza soseji.

ii) Kufungasha bidhaa zote za nyama zilizochakatwa na kuzikabidhi kwa mtunza stoo kwa maandishi (parking ledger)

iii) Kufanya usafi kwenye maeneo yote ya uzalishaji pamoja na mitambo yote yaani vitendea kazi.

iv) Kujaza taarifa kwenye vitabu vya uzalishaji (Production Ledger).

v) Kufanya jukumu jingine lolote atakalopangiwa na Mwajiri.

### 3.2 SIFA ZA MWOMBAJI.

i) Awe na Astashahada katika fani ya Sayansi ya chakula na Uzalishaji,Cheti cha uchakataji nyama au sifa sawa na hizo kutoka chuo kinachotambuliwa na Serikali.

ii) Mwenye uzoefu usiopungua mwaka mmoja (1) katika fani hiyo atapewa kipaumbele.

iii) Awe na umri usiozidi miaka 45.

### 3.3 MSHAHARA.

Kwa kuzingatia ngazi ya mishahara ya Arusha Meat Company Limited yaani ngazi ya **AMCL 2.**

### MASHARTI YA JUMLA KWA NAFASI ILIYOTANGAZWA.

i) Waombaji wawe raia wa Tanzania.

ii) Waombaji waambatanishe Cheti cha kuzaliwa.

iii) Waombaji waambatanishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed C.V) yenye anuani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (referees) watatu pamoja na barua iliyoandikwa kwa mkono na kusainiwa.

iv) Anuani na namba ya simu ya mwombaji na picha moja "Passport size" ya hivi karibuni iandikwe jina kwa nyuma.

v) Maombi yote yaambatane na nakala za vyeti vya taaluma, nakala za vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika vyeti vya kitaaluma (professional certificate) kutoka bodi husika na viwe "Certified".

vi) "Testimonials", "provisional results", "statement of result" hati ya matokeo ya kidato cha nne na sita **HAVITAKUBALIWA.**

vii) Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na mamlaka husika (TCU, NECTA, NACTE).

viii) Mwombaji atajigharamia mwenyewe wakati wa usaili.

ix) Maombi yatakayowasilishwa nje ya utaratibu ulioainishwa katika tangazo hili **HAYATAPOKELEWA.**

x) Ajira hii ni ya mkataba wa muda maalum.

xi) Barua zote zielekezwe kwa;

MENEJA MKUU,

ARUSHA MEAT CO. LTD,

S.L.P 14167,

**ARUSHA-TANZANIA.**

xii) Barua zote za maombi zitumwe kwa njia ya Posta au kwa njia ya barua pepe (email) **recruitment@arushameat.co.tz.**

xiii) Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe 25/09/2025.

**NB: Barua zote zitakazotumwa nje ya utaratibu huu uliolekezwa katika tangazo hili hazitafanyiwa kazi.**

Tangazo hili limetolewa na: -

JONAS E. AYO

**KAIMU MENEJA MKUU**

ARUSHA MEAT CO. LTD

GENERAL MANAGER ★ ARUSHA MEAT COMPANY LIMITED ★ P.O. Box 14167 ARUSHA - TANZANIA